

Majadiliano ya Wadau Kuhusu Agenda ya Maendeleo Baada ya Malengo ya Milenia – 2015

1 Utangulizi

Kama ambavyo mwezeshaji atasisitiza, kabla ya kuanza majadiliano, kila kikundi kinatakiwa kuchagua Mwenyekiti na Katibu ambao wana uelewa mpana zaidi wa mada zinazojadiliwa. Mwenyekiti ndiye atakayeendesha majadiliano kwa kumpa kila mjumbe nafasi sawa ya kuchangia. Katibu atachukua kumbukumbu zote za majadiliano ya kikundi, na viongozi hao watatakiwa kuwasilisha kumbukumbu hizo katika mkutano wa wadau wote. Kila mjumbe wa kikundi ana haki sawa ya kuongea na kutoa mawazo yake kwa uhuru. Wawezeshaji watakuwa karibu sana na kikundi na hivyo viongozi wa kikundi wanashauriwa kuwasiliana na wawezeshaji muda wote linapojitokeza tatizo.

2 Maswali ya Kuongoza Majadiliano ya Vikundi

Maswali yamepangwa katika makundi matano kama ifuatavyo. Kuna maswali yanayohusu NINI? KWA NINI? NANI? KWA VIPI? na LINI?

2.1 NINI?

1 Mtu maskini ana sifa zipi?

2 Makundi yapi ya watu (watu wa aina gani) hawaishi maisha mazuri katika jamii utokayo?

3 Ni kitu gani kimeyafanya maisha ya watu kuwa mazuri au kuwa mabaya siku za karibuni, na nini unadhani kifanyike kurekebisha hali ya kutoishi maisha mazuri? Katika kulifanikisha hilo, wewe unafaa kuwa na wajibu gani? –

➤ **Baada ya kuoredhesha sababu za maisha kuwa mazuri au mabaya wasilisha tatu unazooka ni muhimu zaidi. Pia nini kifanyike taja njia tatu**

4 Je kuna vitu muhimu ambavyo baadhi ya watu wanavikosa katika jamii unayotoka?

➤ **Orodhesha vitatu ambavyo ni muhimu zaidi**

5 Mambo gani yanatakiwa kufanyika ili kuviwezesha vizazi vijavyo kuishi vizuri hapa nchini au katika jamii unayotoka?

➤ **Orodhesha mambo matatu ambayo ndiyo muhimu zaidi**

6 Ni mambo yapi katika jamii unayotoka unadhani ni muhimu kuyahifadhi (au kuyaendeleza) ili kuwawezesha watu kuishi maisha mazuri?

➤ **Orodhesha mambo matatu ambayo ndiyo muhimu zaidi**

2.2 KWA NINI?

1 Sababu zipi kubwa zinazofanya baadhi ya watu wasiwe na maisha mazuri hapa nchini au katika jamii unayotoka? (Ni vizuri majibu yakawa (yakaambatanishwa na) na ushahidi pale inapowezekana).

➤ Orodhesha sababu kuu tatu

2 Je tofauti kati ya wale wanaoishi vizuri na wale wasioishi vizuri hapa nchini inaongezeka au inapungua? Unadhani ni kwa nini?

➤ Toa sababu kuu tatu

2.3 NANI?

1 Kitu gani kifanyike (na watu binafsi au jamii) kuwezesha watu kuishi maisha bora?

➤ Orodhesha yote lakini taja 3 yaliyo muhimu zaidi

2 Ni watendaji wepi au taasisi zipi hapa nchini wanahitaji kufanya kitu (kutenda) kufanikisha watu kuishi maisha bora?

3 Ni watendaji wepi au taasisi zipi nje ya nchi wanahitaji kufanya kitu (kutenda) kufanikisha watu kuishi maisha bora?

2.4 KWA VIPI?

1 Ni vitu gani hao watendaji na taasisi wanatakiwa kufanya?

➤ Taja vitu vikuu vitatu

2 Wanahitaji nini ili waweze kutekeleza hivyo vitu?

➤ Taja mambo makuu matatu

3 Ni namna gani nzuri mabadiliko yanaweza kutokea?

➤ Taja namna 3

2.5 LINI?

1 Ni lini tunahitaji kufanikisha hayo mabadiliko?

2 Tutajuaje kuwa hayo mabadiliko yametokea au hayajatokea?

3 Ni kwa namna gani utaratibu uliotumika kukusanya maoni ya wadau unaweza kutumika kutathmini maendeleo siku za baadae?

Mwisho